

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

Fasihi

Julai/Agosti 2013

MUDA : SAA 2 ½

MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA YA SHULE ZA WILAYA YA NDHIWA

Hati ya kuhitimu kisomo Kenya (K.C.S.E)

Kiswahili

Karatasi 3

Julai/ Agosti

Muda: Saa 2 ½

MAAGIZO:

- *Andika **jina lako** na **nambari yako** katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*
- *Jibu maswali **manne pekee**.*
- *Swali la **kwanza ni lazima**.*
- *Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizosalia yaani; (Riwaya, Hadithi fupi, Ushairi na fasihi simulizi.*
- *Usijibu maswali **mawili** kutoka sehemu moja*

Karatasi hii ina kurasa 4 zilizopigwa chapa. Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

SEHEMU A: RIWAYA

Utengano – Said A. Mohamed

- 1) “Pesa iweke mbele; pesa mwanzo. Sisi tuna msemu wetu watose, ndio watose maana sisi tumeshatoswa.”
 - a) Liweke dondoo hili katika muktadha wake. (ala. 4)
 - b) Eleza mawaidha **mawili** ambayo msemaji alimpa msemewa katika muktadha huu (ala. 4)
 - c) Maisha ya Maimuna yalijaa visiki vya kila aina. Thibitisha kwa mifano mabalimbali kutoka riwaya ya *Utengano*. (ala. 12)

SEHEMU B: TAMTHILIA

Mstahiki Meya – T. Arege

Jibu swali la 2 au 3

- 2) “Nanyi vilevile msikate tamaa. Endeleeni kushinikiza kumwona Meya. Mlango hatimaye huenda ukasalimu armi.”
 - a) Weka dondoo hili haya katika muktadha wake. (ala. 4)
 - b) Taja kwa kutoa mifano; tamathali zozote **mbili** za lugha zilizotumika katika dondoo hili. (ala. 4)
 - c) Kwa kurejelea hoja **sita**, eleza ni kwa nini wanaorejelewa wanakaribia kukata tamaa. (ala. 12)
3. Viongozi katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* wanaonyesha kutowajibika kwa hali ya juu. Eleza (ala. 20)

SEHEMU C: HADITHI FUPI

Damu Nyeusi na Hadhithi Nyinginezo – S.A Mohamed

Jibu swali la 4 au 5

4. “Mimi nilitaka mke, mwanamke mbichi nimvumbike mwenyewe mpaka aive.”
 - a) Weka dondoo hili haya katika muktadha wake (ala. 4)
 - b) Ni kwa nini msemaji alitaka amvumbike mwanamke mwenyewe? (ala. 4)
 - c) Eleza migogoro iliyochipuka baina ya msemaji na mwanamke huyu. (ala. 12)
5. ‘Damu nyeusi’ na ‘Damu nyeupe,’ hazitangamani.
Fafanua kwa mifano ufaafu wa maelezo haya kulingana na Damu Nyeusi. (ala. 20)

SEHEMU YA D: USHAIRI

6. *Soma shairi na kisha uyajibu maswali yanayofuata.*

(Abdalla Abdilalif, sauti ya dhiki)

Chema hakidumu, kingapendekeza,

Saa ikitimu, **kitakuteleza**,

Ukawa na hamu, kuingojeleza,

Huwa ni vigumu, kamwe hutaweza.

Chema sikiimbi, kwamba nakitweza,

Japo mara tumbi, kinshaniliza,

Na japo siombi, kipate n'ongeza,

Mtu haniambi, pa kujikimbiza.

Chema mara ngapi, kin'niondoka,

Mwanangu yu wapi? Hakukaa mwaka,

Kwa muda mfupi, aliwatilika,

Ningefanya lipi, ela kumzika?

Chema wangu babu, kibwana Bashee,

Alojipa tabu, kwamba anilee,

Na yakwe sababu, ni nitengenee,

Ilhali wahhabu, mara amtwee.

Chema wangu poni, kipenzi nyanyangu,

Hadi siku hini, yu moyoni mwangu,

Yu moyoni ndani, hadi kufa kwangu,

Ningamtamani, hatarudi kwangu.

Maswali

- a) Lipe shairi hili anwani mwafaka (al. 2)
- b) Eleza bahari **mbili** zinazojitokeza katika shairi hili (al. 4)
- c) Ni nini maudhui ya shairi hili? (al. 2)

- d) Onyesha matumizi ya aina **tatu** za uhuru wa ushairi (al. 3)
- e) Eleza umbo la beti mbili za mwisho. (al. 4)
- f) Taja na kuonyesha tamathali **mbili** za lugha zilizoko kwenye shairi hili. (al. 2)

- g) Fafanua msamiati huu kwa muktadha wa shairi hili (al. 3)
- i) Kitakuteleza
 - ii) Kinshaniliza
 - iii) ela.

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

7. Taja sifa za tanzu zifuatazo za fasihi simulizi
- i) Ngomezi (al. 5)
 - ii) miviga (al. 5)
 - b) Eleza njia zozote **tano** zinazoweza kutumiwa katika kukusanya data ya Fasihi simulizi. (al. 10)

ANSWERS:

Order a copy of answers from www.schoolsnetkenya.com/order-e-copy

NB> We charge Kshs. 100 ONLY to meet website, e-resource compilation and provision costs